11

# TAKWIMU ZA UKATILI NA UDHALILISHAJI WA KIJINSIA ZANZIBAR

## NOVEMBA, 2024

Funded by the European Union

UN WOMEN
United Nations Entity for Gender Equality and the Empowerment of Women

**20 DISEMBA, 2024**

# TOLEO LA TAKWIMU ZA UKATILI NA UDHALILISHAJI WA KIJINSIA - ZANZIBAR KWA MWEZI WA NOVEMBA, 2024

## UTANGULIZI

Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali imeandaa utaratibu wa kuimarisha takwimu za jinsia nchini ikiwemo kukusanya na kuchambua takwimu za matukio ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia.

Toleo hili hutolewa kila mwezi ambalo hutoa muhtasari wa takwimu za maeneo mawili ya uhalifu ambazo ni ukatili na udhalilishaji wa kijinsia. Takwimu hizi zinatolewa kwa kutofautiana kwa kijiografia, kimakundi na kijinsia.

Takwimu za ukatili na udhalilishaji wa kijinsia hutoa taarifa za idadi ya matukioyaliyotokea, aina ya waathirika na hali ya waathirika baada ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia. Takwimu hizo hutoa taarifa kuhusu matukio ambayo yameainishwa katika makundi makuu sita (6).

## LENGO


Lengo kuu la kutolewa toleo hili ni kutoa taarifa za ukatili na udhalilishaji wa kijinsia ndani ya Zanzibar. Taarifa hizi ni muhimu na hutumiwa na wapangaji, watunga sera nawatoa maamuzi.

## MATUKIO YA UKATILI NA UDHALILISHAJI WA KIJINSIA

Jumla ya matukio 136 ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia yameripotiwa mwezi wa Novemba, 2024 ambapo waathirika walikuwa 136. Waathirika wengi walikuwa watoto sawa na asilimia 86.0, wakifuatiwa na wanawake asilimia 9.6 na wanaume asilimia 4.4.


Miongoni mwa watoto (waathirika 117), wasichana walikuwa 100 (asilimia 73.5) na wavulana walikuwa 17 (asilimia 12.5).

**Kielelezo 1.1: Idadi ya Waathirika wa Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia, Novemba 2024**




Idadi ya Matukio ya kubaka yaliyoripotiwa yalikuwa 52, ambapo waathirika 47 walikuwa wasichana na watano (5) walikuwa wanawake. Matukio ya kulawiti yalikuwa tisa (9) ambapo waathirika wote tisa (9) walikuwa wavulana. Matukio ya kuingilia kinyume na maumbile yalikuwa sita (6) ambapo waathirika wote walikuwa wasichana. Matukio ya kutorosha ni 10 ambapo waathirika wote walikuwa wasichana. Matukio ya shambulio la aibu/kukashifu yalikuwa 33 kati ya hayo waathirika 28 walikuwa wasichana, wanne (4) walikuwa wanawake na mmoja (1) alikuwa mvulana. Matukio ya shambulio yalikuwa 26 ambapo waathirika tisa (9 ) walikuwa wasichana, saba (7) walikuwa wavulana, na waathirika wanne (4) walikuwa wanawake na sita (6) walikuwa wanaume.

**Kielelezo 1.2 Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Aina ya Matukio, Novemba, 2024**




Wilaya ya Magharibi "A" imeripotiwa kuwa na matukio mengi ukilinganisha na wilaya nyengine (matukio 39) sawa na asilimia 28.7 ikifuatia wilaya ya Magharibi "B" ambapo yameripotiwa matukio 32 (asilimia 23.5). Wilaya ya Micheweni na Mkoani zimeripotiwa kuwa na idadi ndogo ya matukio, matukio mawili (2) sawa na asilimia 1.5 kwa kila wilaya .

**Kielelezo 1.3: Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wilaya Novemba, 2024**




Idadi ya matukio kwa mwezi yamepungua kwa asilimia 7.5 kufikia matukio 136 mwezi wa Novemba, 2024 kutoka matukio 147 kwa mwezi wa Oktoba 2024. Aidha, matukio ya kuingilia kinyume na maumbile na shambulio la aibu/kukashifu yameripotiwa kuongezeka kwa mwezi wa Novemba 2024.

Wilaya ya Magahribi “A” imeripotiwa kuwa na matukio mengi ikilinganishwa na wilaya nyengine (matukio 39) kwa mwezi wa Novemba, 2024 na wilaya ya Magahribi “B” iliongoza kwa mwezi wa Oktoba , 2024 (matukio 37).

**Jadweli 1.1: Mlinganisho wa Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wilaya Oktoba, 2024 na Novemba, 2024**

| Wilaya | Idadi ya Matukio | | Aina ya Ukatili na Udhalilishaji | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Kubaka | | Kulawiti | | Kuingilia Kinyume na Maumbile | | Kutorosha | | Shambulio la Aibu/Kukashifu | | Shambulio | |
| | Oktoba 2024 | Novemba 2024 | Oktoba 2024 | Novemba 2024 | Oktoba 2024 | Novemba 2024 | Oktoba 2024 | Novemba 2024 | Oktoba 2024 | Novemba 2024 | Oktoba 2024 | Novemba 2024 | Oktoba 2024 | Novemba 2024 |
| Kaskazini 'A' | 5 | 4 | 3 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 1 | 0 | 0 |
| Kaskazini 'B' | 7 | 5 | 7 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 3 | 0 | 0 |
| Kati | 6 | 6 | 5 | 6 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| Kusini | 4 | 5 | 2 | 3 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 2 | 0 | 0 | 0 |
| Mjini | 32 | 26 | 7 | 7 | 4 | 2 | 1 | 2 | 3 | 0 | 7 | 4 | 10 | 11 |
| Magharibi 'A' | 31 | 39 | 8 | 8 | 3 | 4 | 1 | 2 | 3 | 2 | 6 | 14 | 10 | 9 |
| Magharibi 'B' | 37 | 32 | 10 | 15 | 2 | 2 | 0 | 1 | 10 | 2 | 6 | 6 | 9 | 6 |
| Wete | 10 | 5 | 5 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 3 | 2 | 2 | 1 | 0 | 0 |
| Micheweni | 5 | 2 | 3 | 2 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| Chake Chake | 5 | 10 | 1 | 5 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 2 | 2 | 3 | 0 | 0 |
| Mkoani | 5 | 2 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 1 | 2 | 1 | 0 | 0 |
| **Zanzibar** | **147** | **136** | **53** | **52** | **11** | **9** | **2** | **6** | **21** | **10** | **31** | **33** | **29** | **26** |

Idadi ya matukio kwa mwaka yamepungua kwa asilimia 20.9 kufikia matukio 136 kwa mwezi Novemba, 2024 kutoka matukio 172 kwa mwezi wa Novemba, 2023. Tukio la shambulio la aibu/kukashifu limeripotiwa kuongezeka kwa mwezi Novemba, 2024. Wilaya ya Magharibi “A” imeongoza kwa idadi kubwa ya matukio kwa Novemba, 2024 (matukio 39) na wilaya ya Magharibi “B” iliongoza kwa mwezi wa Novemba, 2023 (matukio 47).

**Jadweli 1.2: Mlinganisho wa Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wilaya na Aina ya udhalilishaji, Novemba 2023 na Novemba, 2024**

| Wilaya | Idadi ya Matukio | | Aina ya Ukatili na Udhalilishaji | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Kubaka | | Kulawiti | | Kuingilia Kinyumena Maumbile | | Kutorosha | | Shambulio la Aibu/Kukashifu | | Shambulio | |
| | Nov 2023 | Nov 2024 | Nov 2023 | Nov 2024 | Nov 2023 | Nov 2024 | Nov 2023 | Nov 2024 | Nov 2023 | Nov 2024 | Nov 2023 | Nov 2024 | Nov 2023 | Nov 2024 |
| Kaskazini 'A' | 6 | 4 | 3 | 3 | 1 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 |
| Kaskazini 'B' | 6 | 5 | 6 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 3 | 0 | 0 |
| Kati | 8 | 6 | 3 | 6 | 1 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 |
| Kusini | 3 | 5 | 1 | 3 | 1 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| Mjini | 42 | 26 | 14 | 7 | 9 | 2 | 2 | 2 | 1 | 0 | 1 | 4 | 15 | 11 |
| Magharibi 'A' | 35 | 39 | 15 | 8 | 3 | 4 | 1 | 2 | 1 | 2 | 7 | 14 | 8 | 9 |
| Magharibi 'B' | 47 | 32 | 22 | 15 | 6 | 2 | 6 | 1 | 2 | 2 | 2 | 6 | 9 | 6 |
| Wete | 4 | 5 | 2 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 2 | 2 | 0 | 1 | 0 | 0 |
| Micheweni | 2 | 2 | 1 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Chake Chake | 13 | 10 | 7 | 5 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 2 | 5 | 3 | 0 | 0 |
| Mkoani | 6 | 2 | 6 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 |
| **Zanzibar** | **172** | **136** | **80** | **52** | **21** | **9** | **11** | **6** | **10** | **10** | **18** | **33** | **32** | **26** |

Miongoni mwa watoto 117 waathirika wa ukatili na udhalilishaji wa kijinsia; Wasichana waliobakwa walikuwa 47, Wavulana waliolawitiwa walikuwa tisa (9), Kuingilia kinyume na maumbile walikuwa wasichana sita (6), Kutorosha walikuwa wasichana 10, shambulio la aibu/kukashifu walikuwa 29 ambapo 28 walikuwa wasichana na mmoja(1) alikuwa mvulana na shambulio walikuwa 16 kati yao wasichana walikuwa tisa(9) na wavulana walikuwa saba(7).

**Jadweli 1.3: Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Watoto, Wilaya na Aina ya Matukio Novemba, 2024**

| Wilaya | Idadi ya Matukio | Aina ya Ukatili na Udhalilishaji Zanzibar | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Kubaka | Kulawiti | Kuingilia Kinyume na Maumbile | Kutorosha | | Shambulio la Aibu/Kukashifu | | Shambulio | |
| | | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wavulana |
| Kaskazini 'A' | 2 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| Kaskazini 'B' | 4 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 |
| Kati | 6 | 6 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kusini | 5 | 3 | 0 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mjini | 21 | 7 | 2 | 2 | 0 | 0 | 4 | 0 | 4 | 2 |
| Magharibi 'A' | 32 | 7 | 4 | 2 | 2 | 0 | 12 | 0 | 3 | 2 |
| Magharibi 'B' | 30 | 15 | 2 | 1 | 2 | 0 | 5 | 0 | 2 | 3 |
| Wete | 5 | 1 | 1 | 0 | 2 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| Micheweni | 2 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Chake Chake | 8 | 3 | 0 | 0 | 2 | 0 | 2 | 1 | 0 | 0 |
| Mkoani | 2 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| **Zanzibar** | **117** | **47** | **9** | **6** | **10** | **0** | **28** | **1** | **9** | **7** |

Miongoni mwa wanawake 13 waathirika wa ukatili na udhalilishaji wa kijinsia; wanawake waliobakwa walikuwa watano(5), Shambulio la aibu/Kukashifu walikuwa wanane (4) na shambulio walikuwa wanawake wanne (4).

**Jadweli 1.4a: Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wanawake kwa Wilaya Novemba, 2024**

| Wilaya | Idadi ya Matukio | Aina ya Ukatili na Udhalilishaji | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Kubaka | Kuingilia Kinyumena Maumbile | Kutorosha | Shambulio la Aibu/Kukashifu | Shambulio |
| Kaskazini 'A' | 2 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kaskazini 'B' | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| Kati | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kusini | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mjini | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 |
| Magharibi 'A' | 5 | 1 | 0 | 0 | 2 | 2 |
| Magharibi 'B' | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| Wete | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Micheweni | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Chakechake | 2 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mkoani | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Zanzibar** | **13** | **5** | **0** | **0** | **4** | **4** |

Jumla ya wanaume sita(6) walioripotiwa kufanyiwa ukatili na udhalilishaji wa kijinsia, wote waliripotiwa kufanyiwa shambulio ambapo walikuwa wanaume sita (6).

**Jadweli 1.4b: Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wanaume kwa Wilaya Novemba, 2024**

| Wilaya | Idadi ya Matukio | Aina ya Ukatili na Udhalilishaji | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Kulawiti | Kutorosha | Shambulio la Kukashifu | Shambulio |
| Kaskazini 'A' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kaskazini 'B' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kati | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kusini | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mjini | 3 | 0 | 0 | 0 | 3 |
| Magharibi 'A' | 2 | 0 | 0 | 0 | 2 |
| Magharibi 'B' | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 |
| Wete | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Micheweni | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Chakechake | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mkoani | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Zanzibar** | **6** | **0** | **0** | **0** | **6** |

Watoto wenye umri wa miaka 15-17 wameripotiwa kuwa na idadi kubwa ya matukio (matukio 54) sawa na asilimia 46.2 ya matukio yote ya watoto yaliyoripotiwa ikifuatiwa na umri wa miaka 11-14 (matukio 36) sawa na asilimia 30.8. Aidha matukio ya kubaka yanaonesha kuwa mengi zaidi katika umri wa miaka 15-17 (matukio 28) sawa na asilimia 59.6 kati ya matukio yote ya kubaka yalioripotiwa.

**Jadweli 1.5: Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Watoto na Umri Novemba, 2024**

| Miaka | Aina ya Ukatili naUdhalilishaji | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Kubaka | | Kulawiti | | Kuingilia Kinyume na Maumbile | | Kutorosha | | Shambulio la Aibu/Kukashifu | | Shambulio | | Jumla |
| | Wavulana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | |
| 0-5 | | 0 | 0 | | | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 2 |
| 6-10 | | 6 | 3 | | | 0 | 0 | 0 | 0 | 12 | 2 | 2 | 25 |
| 11-14 | | 13 | 4 | | | 2 | 0 | 2 | 1 | 8 | 3 | 3 | 36 |
| 15-17 | | 28 | 2 | | | 3 | 0 | 8 | 0 | 7 | 2 | 4 | 54 |
| **Jumla** | | **47** | **9** | | | **6** | **0** | **10** | **1** | **28** | **7** | **9** | **117** |

Idadi ya watoto waathirika wa matukio ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia kwa mwezi wa Novemba, 2024 yamepungua kwa asilimia 4.1 kufikia matukio 117 kwa mwezi wa Novemba 2024 kutoka 122 kwa mwezi wa Oktoba 2024. Mlinganisho wa idadi ya watoto waathirika kwenye umri wa miaka 11-14 yameripotiwa kuwa sawa kwa mwezi wa Novemba 2024 na Oktoba 2024.

**Jadweli 1.6: Mlinganisho wa Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Watoto kwa Umri, Oktoba 2024 na Novemba 2024**

| Miaka | Aina ya Ukatili na Udhalilishaji | | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Kubaka | | Kulawiti | | Kuingilia Kinyume na Maumbile | | Kutorosha | | Shambulio la Aibu/Kukashifu | | Shambulio | | Jumla | |
| | Oktoba 2024 | Novemba 2024 | Oktoba 2024 | Novemba 2024 | Oktoba 2024 | Novemba 2024 | Oktoba 2024 | Novemba 2024 | Oktoba 2024 | Novemba 2024 | Oktoba 2024 | Novemba 2024 | Oktoba 2024 | Novemba 2024 |
| 0-5 | 2 | 0 | 2 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 5 | 1 | 0 | 0 | 9 | 2 |
| 06 -10 | 1 | 6 | 6 | 3 | 2 | 0 | 0 | 0 | 5 | 12 | 5 | 4 | 19 | 25 |
| 11 -14 | 11 | 13 | 3 | 4 | 0 | 2 | 7 | 2 | 10 | 9 | 5 | 6 | 36 | 36 |
| 15-17 | 31 | 28 | 0 | 2 | 0 | 3 | 14 | 8 | 6 | 7 | 7 | 6 | 58 | 54 |
| **Jumla** | **45** | **47** | **11** | **9** | **2** | **6** | **21** | **10** | **26** | **29** | **17** | **16** | **122** | **117** |


Idadi ya matukio ya watoto kwa mwaka yamepungua kwa asilimia 20.4 kufikia matukio 117 kwa mwezi wa Novemba 2024 kutoka matukio 147 kwa mwezi wa Novemba 2023. Mlinganisho wa idadi ya watoto waathirika kwenye umri wa miaka kuanzia sita (6) hadi 14 yameongezeka kwa mwezi Novemba , 2024.

**Jadweli 1.7: Mlinganisho wa Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Watoto kwa Umri na Aina ya Matukio, Mwezi Novemba, 2023 na Novemba, 2024**

| | Aina ya Ukatili na Udhalilishaji | | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Miaka | Kubaka | | Kulawiti | | Kuingilia Kinyume na Maumbile | | Kutorosha | | Shambulio la Aibu/Kukashifu | | Shambulio | | Jumla | |
| | Nov 2023 | Nov 2024 | Nov 2023 | Nov 2024 | Nov 2023 | Nov 2024 | Nov 2023 | Nov 2024 | Nov 2023 | Nov 2024 | Nov 2023 | Nov 2024 | Nov 2023 | Nov 2024 |
| 0-5 | 4 | 0 | 2 | 0 | 1 | 1 | 0 | 0 | 2 | 1 | 0 | 0 | 9 | 2 |
| 6-10 | 3 | 6 | 3 | 3 | 2 | 0 | 0 | 0 | 9 | 12 | 2 | 4 | 19 | 25 |
| 11-14 | 16 | 13 | 6 | 4 | 2 | 2 | 1 | 2 | 3 | 9 | 7 | 6 | 35 | 36 |
| 15-17 | 49 | 28 | 10 | 2 | 4 | 3 | 9 | 8 | 2 | 7 | 10 | 6 | 84 | 54 |
| **Jumla** | **72** | **47** | **21** | **9** | **9** | **6** | **10** | **10** | **16** | **29** | **19** | **16** | **147** | **117** |

Matukio mengi (matukio 56) yametokea sehemu nyengine (vichakani na kwengine) sawa na asilimia 41.2 ikifuatiwa na matukio yaliyotokea nyumbani kwa mtuhumiwa (matukio 51) sawa na asilimia 37.5 ikilinganishwa na maeneo mengine yaliyotajwa.

**Kielelezo 1.4: Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia na Sehemu Yaliyotokea Novemba, 2024**





Matukio 114 kati ya matukio 136 yaliyoripotiwa yapo chini ya upelelezi wa Jeshi la Polisi sawa na asilimia 83.8. Aidha, matukio 21 yapo Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka sawa na asilimia 15.4 na tukio moja (1) limefungwa na polisi( asilimia 0.7) .

**Jadweli 1.8: Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia na Hatua Zilizochukuliwa Novemba, 2024**

| | | Waliofanyiwa ukatili na udhalilishaji | | | | Hatua zilizochukuliwa | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Aina ya makosa | Idadi ya makosa | Watu wazima | | Watoto | | Zilizo Mahakaman | Zilizotiwa hatiani | Ziliachiwa huru | Zilizofungwa Polisi | Zilizopelekwa kwa Offisi ya M' mashtaka | Zilizo chini ya Upelelezi |
| | | Wanaume | Wanawake | M'me | M'ke | | | | | | |
| Kubaka | 52 | [redacted] | 5 | [redacted] | 47 | 0 | 0 | 0 | 0 | 5 | 47 |
| Kulawiti/Kunajis | 9 | 0 | [redacted] | 9 | [redacted] | 0 | 0 | 0 | 0 | 3 | 6 |
| Kuingilia kinyume na maumbile | 6 | [redacted] | 0 | [redacted] | 6 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 6 |
| Kutorosha | 10 | 0 | 0 | 0 | 10 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 9 |
| Shambulio la aibu/Kukashifu | 33 | 0 | 4 | 1 | 28 | 0 | 0 | 0 | 1 | 5 | 27 |
| Shambulio | 26 | 6 | 4 | 7 | 9 | 0 | 0 | 0 | 0 | 7 | 19 |
| **Jumla** | **136** | **6** | **13** | **17** | **100** | **0** | **0** | **0** | **1** | **21** | **114** |

Wafanyaji wa matukio ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia walioripotiwa kwa mwezi wa Novemba, 2024 walikuwa 136 kati yao, 90 walikuwa wapita njia sawa na asilimia 66.2 , jirani walikuwa 43 sawa na asilimia 31.6, Wapenzi walikuwa wawili (2) asilimia 1.5 na Mkulima alikuwa mmoja sawa na asilimia 0.7

**Kielelezo 1.5: Aina ya Watu Waliofanya Matukio ya Ukatiki na Udhalilishaji wa Kijinsia Novemba, 2024**



## MAJALADA YA MAKOSA YA UDHALILISHAJI YALIYOPOKELEWA AFISI YA MKURUGENZI WA MASHTAKA ZANZIBAR NOVEMBA, 2024

Jumla ya Majalada 80 yamepokelewa Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kwa mwezi wa Novemba, 2024 ambayo yalihusisha makosa 94.

Idadi kubwa ya makosa yaliyopokelewa yametokea Mkoa wa Mjini Magharibi (makosa 72) sawa na asilimia 76.6 ya makosa yote ikilinganishwa na mikoa mwengine.

**Jadweli 2.1: Idadi ya Majalada na Mkosa ya Udhalilishaji Yaliyopokelewa Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kwa Mkoa Novemba,2024**

| Mkoa | Idadi ya Majalada | Idadi ya Makosa |
|---|---|---|
| Kaskazini Unguja | 8 | 8 |
| Kusini Unguja | 7 | 7 |
| Mjini Magharibi | 58 | 72 |
| Kaskazini Pemba | 4 | 4 |
| Kusini Pemba | 3 | 3 |
| Makao Makuu | 0 | 0 |
| **Jumla** | **80** | **94** |

Kati ya Majalada 80 yaliyopokelewa, majalada tisa (9) yamependekezwa kufungwa, majalada 26 yamerudishwa Polisi kwa Upelelezi zaidi, majalada 30 yameruhusiwa kwenda mahakamani na majalada 15 hayajatolewa uamuzi.

**Jadweli 2.2: Majalada ya Makosa ya Udhalilishaji Yaliyopokelewa Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kwa Mkoa na Hatua, Novemba 2024**

| Mkoa | Idadi ya Majalada | Yalio ruhusiwa kwenda Mahakamani | Yalio Pendekezwa kufungwa | Yalio rudi Polisi kwa Upelelezi | Hayajatolewa Uamuzi |
|---|---|---|---|---|---|
| Kaskazini Unguja | 8 | 2 | 0 | 0 | 6 |
| Kusini Unguja | 7 | 6 | 1 | 0 | 0 |
| Mjini Magharibi | 58 | 17 | 8 | 24 | 9 |
| Kaskazini Pemba | 4 | 2 | 0 | 2 | 0 |
| Kusini Pemba | 3 | 3 | 0 | 0 | 0 |
| Mkao Makuu | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **80** | **30** | **9** | **26** | **15** |

Miongoni mwa makosa 94 ya udhalilishaji yaliyopokelewa Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka, makosa mengi zaidi yaliyojitokeza yanahusiana na kubaka (makosa 53) sawa na asilimia 56.4 ya makosa yote yaliyopokelewa.


**Jadweli 2.3: Idadi ya Makosa ya Udhalilishaji Yaliyopokelewa Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kwa Mkoa, Novemba 2024**

| Mkoa | Idadi ya Makosa | Kubaka | Kuingilia Kinyume na Maumbile | Kulawiti/Kunajis | Kutorosha | Shanbulio la Aibu/Kukashifu | Kubaka kwa kundi | Shambulio | Ukatili wa Mtoto | Kumwingilia Maharimu | Uzinifu |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Kaskazini Unguja | 8 | 6 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kusini Unguja | 7 | 5 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mjini Magharibi | 72 | 36 | 8 | 9 | 6 | 3 | 0 | 1 | 1 | 7 | 1 |
| Kaskazini Pemba | 4 | 4 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kusini Pemba | 3 | 2 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Makao Makuu | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **94** | **53** | **9** | **13** | **6** | **3** | **0** | **1** | **1** | **7** | **1** |

## TAKWIMU ZA UDHALILISHAJI ZILIZOFUNGULIWA KATIKA MAHKAMA ZA UDHALILISHAJI ZANZIBAR KWA MWEZI WA NOVEMBA 2024

Jumla ya mashauri 15 yamefunguliwa katika mahkama za udhalilishaji kwa mwezi wa Novemba, 2024 ambapo Mkoa wa Mjini Magharibi umeripotiwa kuwa na mashauri mengi yaliyofunguliwa (mashauri 9) sawa na asilimia 60.0 ikilinganishwa na mikoa mengine.

**Kielelezo 3.1: Mashauri Yaliyofunguliwa kwa Mkoa Novemba, 2024**




Jumla ya mashauri yaliyofunguliwa katika Mahkama za udhalilishaji Zanzibar yalikuwa15, ambapo mashauri yote 15 bado yanaendelea.

**Jadweli 3.1: Mashauri Yaliyofunguliwa katika Mahkama za Udhalilishaji kwa Hatua na Aina ya Kosa Novemba, 2024**

| Aina ya Kosa | Zilizofunguliwa | Zilizotolewa uamuzi | | | Zinazoendelea |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Huru | Kufutwa | Faini | |
| Kubaka | 9 | 0 | 0 | 0 | 9 |
| Kulawiti | 2 | 0 | 0 | 0 | 2 |
| Shambulio la Aibu/Kukashifu | 3 | 0 | 0 | 0 | 3 |
| Kutorosha | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kuingilia Kinyume na Maumbile | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 |
| Kubaka Mgonjwa wa akili | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **15** | **0** | **0** | **0** | **15** |

Jumla ya washtakiwa wa makosa ya vitendo vya udhalilishaji walikuwa 15 ambapo washtakiwa wote walikuwa wanaume. Washtakiwa wengi zaidi walikuwa na umri wa miaka 14-17 na 34-37 (washtakiwa 5 kwa kila kundi la umri) sawa na asilimia 33.3

Jumla ya waathirika wa vitendo vya udhalilishaji walikuwa 15 ambapo waathirika wawili (2) walikuwa wavulana na waathirika 13 walikuwa wasichana na wanawake. Waathirika wengi zaidi walikuwa na umri wa miaka 15-19 (waathirika 8) sawa na asilimia 53.3.

**Jadweli 3.2: Idadi ya Washtakiwa na Waathirika wa Vitendo vya Udhalilishaji katika Mahkama za Udhalilishaji kwa Jinsi na Umri Novemba, 2024**

| Umri wa Mshtakiwa | Washtakiwa | | Umri wa Waathirika | Waathirika | |
|---|---|---|---|---|---|
| | M/ME | MKE | | M/ME | MKE |
| 14-17 | 5 | 0 | 0-4 | 0 | 0 |
| 18-21 | 4 | 0 | 5-9 | 0 | 0 |
| 22-25 | 1 | 0 | 10-14 | 2 | 5 |
| 26-29 | 0 | 0 | 15-19 | 0 | 8 |
| 30-33 | 0 | 0 | 20-24 | 0 | 0 |
| 34-37 | 5 | 0 | 25-29 | 0 | 0 |
| 38-41 | 0 | 0 | 30-34 | 0 | 0 |
| 42-45 | 0 | 0 | 35-39 | 0 | 0 |
| 46-49 | 0 | 0 | 40-49 | 0 | 0 |
| 50+ | 0 | 0 | 50+ | 0 | 0 |
| **Jumla** | **15** | **0** | **Jumla** | **2** | **13** |

## HITIMISHO

Takwimu za ukatili na udhalilishaji wa kijinsia hutoa taarifa za idadi ya matukio yaliyotokea, aina ya waathirika na hali ya waathirika baada ya ukatili na udhalilishaji wa Kijinsia, muda wa matukio yalipotokea na wafanyaji wa matukio. Takwimu hizo hutoa taarifa kuhusu matukio ambayo yameainishwa katika makundi makuu sita (6). Lengo kuu la kutolewa toleo hili ni kutoa taarifa za ukatili na udhalilishaji wa kijinsia za ndani ya Zanzibar. Taarifa hizi ni muhimu na hutumiwa na wapangaji, watunga sera na watoa maamuzi.

Jumla ya matukio 136 ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia yameripotiwa mwezi wa Novemba, 2024 ambapo waathirika walikuwa 136. Wilaya ya Magharibi "A" imeripotiwa kuwa na matukio mengi ukilinganisha na wilaya nyengine (matukio 39) sawa na asilimia 28.7 . Idadi ya matukio kwa mwezi yamepungua kwa asilimia 7.5 kufikia matukio 136 mwezi wa Novemba, 2024 kutoka matukio 147 kwa mwezi wa Oktoba, 2024.

Matukio 114 kati ya matukio 136 yaliyoripotiwa yapo chini ya upelelezi wa Jeshi la Polisi sawa na asilimia 83.8, matukio 21 yapo Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka sawa na asilimia 15.4 na tukio moja (1) limefungwa na polisi( asilimia 0.7 )

## Kiambatanisho

**Jadweli 1.0: Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia na Maeneo yaliyofanyika na Aina ya Matukio Novemba, 2024**

| Eneo la matukio | Kubaka | | | Kulawiti | | | Kuingilia kinyume na maumbile | | | Kutorosha | | | Shambulio la aibu/Kukashifu | | | Shambulio | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | W'ke | W'me | Jumla | W'ke | W'me | Jumla | W'ke | W'me | Jumla | W'ke | W'me | Jumla | W'ke | W'me | Jumla | W'ke | W'me | Jumla |
| Nyumbani kwa Muathirika | 0 | [redacted] | 0 | [redacted] | 0 | 0 | 0 | [redacted] | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| Nyumbani kwa Mtuhumiwa | 21 | [redacted] | 21 | [redacted] | 1 | 1 | 2 | [redacted] | 2 | 7 | 0 | 7 | 9 | 0 | 9 | 6 | 5 | 11 |
| Nyumba za wageni/kwa rafiki | 5 | [redacted] | 5 | [redacted] | 0 | 0 | 1 | [redacted] | 1 | 2 | 0 | 2 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| Sehemu za kazi | 0 | [redacted] | 0 | [redacted] | 0 | 0 | 0 | [redacted] | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Skuli/Madrasa | 0 | [redacted] | 0 | [redacted] | 0 | 0 | 0 | [redacted] | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Majumba mabovu | 9 | [redacted] | 9 | [redacted] | 4 | 4 | 1 | [redacted] | 1 | 0 | 0 | 0 | 5 | 0 | 5 | 0 | 0 | 0 |
| Sehemu nyengine(Vichakani na kwengine) | 17 | [redacted] | 17 | [redacted] | 4 | 4 | 2 | [redacted] | 2 | 1 | 0 | 1 | 16 | 1 | 17 | 7 | 8 | 15 |
| **Jumla** | **52** | [redacted] | **52** | [redacted] | **9** | **9** | **6** | [redacted] | **6** | **10** | **0** | **10** | **32** | **1** | **33** | **13** | **13** | **26** |

**Jadweli 1.2: Mlinganisho wa Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia na Maeneo yaliyofanyika Matukio baina ya Mwezi Oktoba, 2024 na Novemba, 2024**

| Eneo la matukio | Kubaka | | Kulawiti | | Kuingilia Kinyumena Maumbile | | Kutorosha | | Shambulio la Aibu/Kukashifu | | Shambulio | | Jumla | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Oktoba 2024 | Novemba 2024 | Oktoba 2024 | Novemba 2024 | Oktoba 2024 | Novemba 2024 | Oktoba 2024 | Novemba 2024 | Oktoba 2024 | Novemba 2024 | Oktoba 2024 | Novemba 2024 | Oktoba 2024 | Nov 2024 |
| Nyumbani kwa Muathirika | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 8 | 1 | 4 | 0 | 12 | 1 |
| Nyumbani kwa Mtuhumiwa | 25 | 21 | 6 | 1 | 2 | 2 | 12 | 7 | 6 | 9 | 10 | 11 | 57 | 51 |
| Nyumba za wageni/kwa rafiki | 4 | 5 | 0 | 0 | 0 | 1 | 2 | 2 | 0 | 1 | 2 | 0 | 7 | 9 |
| Sehemu za kazi | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Skuli | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Madrasa | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 |
| Majumba mabovu | 13 | 9 | 2 | 4 | 0 | 1 | 2 | 0 | 3 | 5 | 2 | 0 | 24 | 19 |
| Sehemu nyengine(Vichakanina kwengine) | 22 | 17 | 7 | 4 | 0 | 2 | 5 | 1 | 12 | 17 | 10 | 15 | 47 | 56 |
| **Jumla** | **64** | **52** | **15** | **9** | **2** | **6** | **21** | **10** | **29** | **33** | **28** | **26** | **147** | **136** |

**Jadweli 2.0: Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wilaya Novemba, 2024**

| Wilaya | Idadi ya Matukio | Aina ya Ukatili na Udhalilishaji Zanzibar | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Kubaka | Kulawiti | Kuingilia Kinyume na Maumbile | Kutorosha | Shambulio la Aibu/Kukashifu | Shambulio |
| Kaskazini 'A' | 4 | 3 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| Kaskazini 'B' | 5 | 2 | 0 | 0 | 0 | 3 | 0 |
| Kati | 6 | 6 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kusini | 5 | 3 | 0 | 1 | 1 | 0 | 0 |
| Mjini | 26 | 7 | 2 | 2 | 0 | 4 | 11 |
| Magharibi 'A' | 39 | 8 | 4 | 2 | 2 | 14 | 9 |
| Magharibi 'B' | 32 | 15 | 2 | 1 | 2 | 6 | 6 |
| Wete | 5 | 1 | 1 | 0 | 2 | 1 | 0 |
| Micheweni | 2 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Chake Chake | 10 | 5 | 0 | 0 | 2 | 3 | 0 |
| Mkoani | 2 | 0 | 0 | 0 | 1 | 1 | 0 |
| **Zanzibar** | **136** | **52** | **9** | **6** | **10** | **33** | **26** |

**Jadweli 3.0: Mlinganisho wa Idadi  ya Matukio na Waathirika wa Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia, baina ya Mwezi Oktoba, 2024 na Novemba, 2024**

| Aina ya matukio | Idadi ya Matukio | | Waathirika | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Wanawake | | Watoto | | | | Wanaume | |
| | | | | | Wasichana | | Wavulana | | | |
| | Oktoba 2024 | Novemba 2024 | Oktoba 2024 | Novemba 2024 | Oktoba 2024 | Novemba 2024 | Oktoba 2024 | Novemba 2024 | Oktoba 2024 | Novemba 2024 |
| Kubaka | 53 | 52 | 8 | 5 | 45 | 47 | | | | |
| Kulawiti | 11 | 9 | | | | | 11 | 9 | 1 | 0 |
| Kuingiliwa kinyume na maumbile | 2 | 6 | 0 | 0 | 2 | 6 | | | | |
| Kutorosha | 21 | 10 | 0 | 0 | 20 | 10 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| Shambulio la aibu/Kukashifu | 31 | 33 | 3 | 4 | 26 | 28 | 0 | 1 | 2 | 0 |
| Shambulio | 29 | 26 | 6 | 4 | 8 | 9 | 9 | 7 | 6 | 6 |
| **Jumla** | **147** | **136** | **17** | **13** | **101** | **100** | **21** | **17** | **8** | **6** |

**Jadweli 4.0: Mlinganisho wa Idadi ya Matukio na Waathirika wa Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia, baina ya Mwezi Novemba, 2023 na Novemba, 2024**

| Aina ya matukio | Idadi ya Matukio | | Waathirika | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Wanawake | | Watoto | | | | Wanaume | |
| | | | | | Wasichana | | Wavulana | | | |
| | Novemba 2023 | Novemba 2024 | Novemba 2023 | Novemba 2024 | Novemba 2023 | Novemba 2024 | Novemba 2023 | Novemba 2024 | Novemba 2023 | Novemba 2024 |
| Kubaka | 80 | 52 | 72 | 5 | 72 | 47 | | | | |
| Kulawiti | 21 | 9 | | | | | 21 | 9 | 0 | 0 |
| Kuingiliwa kinyume na maumbile | 11 | 6 | 9 | 0 | 9 | 6 | | | | |
| Kutorosha | 10 | 10 | 10 | 0 | 10 | 10 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Shambulio la aibu/Kukashifu | 18 | 33 | 12 | 4 | 12 | 28 | 4 | 1 | 0 | 0 |
| Shambulio | 32 | 26 | 9 | 4 | 9 | 9 | 10 | 7 | 7 | 6 |
| **Jumla** | **172** | **136** | **112** | **13** | **112** | **100** | **35** | **17** | **7** | **6** |

**Jadweli 5.0: Idadi ya Waathirika Wanawake wa Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia, kwa Umri na Aina ya Matukio; Novemba 2024**

| Umri | Idadi ya Matukio | Aina ya ukatili na udhalilishaji | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Kubaka | Kuingilia kinyume na maumbile | Kutorosha | Shambulio la aibu/Kukashifu | Shambulio |
| 18-29 | 13 | 5 | 0 | 0 | 4 | 4 |
| 30-39 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 40-49 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 50-59 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 60-69 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70-79 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 80+ | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **13** | **5** | **0** | **0** | **4** | **4** |

**Jadweli 6.0: Idadi ya Waathirika Wanaume wa Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia, kwa Umri na Aina ya Matukio; Novemba 2024**

| Umri | Idadi ya Matukio | Aina ya ukatili na udhalilishaji | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Kulawiti | Kutorosha | Shambulio la aibu/Kukashifu | Shambulio |
| 18-29 | 6 | 0 | 0 | 0 | 6 |
| 30-39 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 40-49 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 50-59 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 60-69 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70-79 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 80+ | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **6** | **0** | **0** | **0** | **6** |

**Jadweli 7.0: Muda wa Matukio ya Udhalilishaji Yalipotokea; Novemba, 2024**

| Muda | Kubaka | Kulawiti/Kunajisi | Kuingilia Kinyume na Maumbile | Kutorosha | Shambulio la Aibu /Kukashifu | Shambulio | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 12:01 - 03:00 Asubuhi | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 |
| 03:01 - 06:00 Mchana | 8 | 1 | 0 | 0 | 7 | 4 | 20 |
| 06:01 - 09:00 Jioni | 3 | 1 | 0 | 0 | 6 | 2 | 12 |
| 09:01 - 12:00 Jioni | 14 | 4 | 3 | 4 | 10 | 7 | 42 |
| 12:01 - 03:00 Usiku | 26 | 3 | 3 | 6 | 9 | 8 | 55 |
| 03:01 - 06:00 Usiku | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 5 | 6 |
| 06:01 - 09:00 Usiku | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 09:01 - 12:00 Asubuhi | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **52** | **9** | **6** | **10** | **33** | **26** | **136** |

## Zingatia Maelezo

Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia Kitendochochote au mwenendo wowote, ambao husababisha moja kwa moja kwa mtu, kama mateso ya kimwili, ya kimapenzi auya kiakili kupitia vitisho, kulazimisha au njia zingine; lengo la kutisha, kuadhibu, kuwadhalilisha, kudhoofisha usalama au kujiheshimu; kutosheleza hamu ya ngono; au kudhoofisha uwezo wa mwili au kiakili wa mtu kwa sababu ya jinsi yake. Kwa mfano, unyanyasaji wa kijinsia, kumpiga mke, unyanyasaji wa kijinsia wa wasichana na wavulana, ukeketaji wa kike, mwanamke kuua watoto wachanga, utoaji mimba, ukahaba wa kulazimishwa , Biashara haramu ya usafirishaji wa wanawake na watoto wa kike na ponografia (uenezaji wangono haramu).

Sheria ya Adhabu ya 6/2018 iliongeza adhabu kwa makosa yanayohusiana na maadili kama vile ubakaji, kulawiti, kuingilia kinyume na kimaumbile nashambulio la aibu;

Sheria hii imetungwa mwaka 2018 ambayo imekuja kufuta sheria kama hiiya mwaka 2004. Sheria hii imetungwapamoja na mambo mengine kuyafanya baadhi ya matendo kuwa makosa ya jinai na kuyawekea adhabu zake endapo mtu yeyote atayatenda matendo hayo na mahkama itamuona ana hatia. Kwenyeshehemu ya kumi na tatu (Section thirteen)ya sheria ya adhabu imejumuisha makosa mengi ambayo ni makosa dhidi ya vitendovya ukatili na udhalilishaji wa wanawake na watoto.

Sheria ya mwenendo wa Jinai 7/2018 kifungu cha 151 (1) kina vifungu ambavyohaviruhusu utoaji wa dhamana kwa mtu yeyote anayeshtakiwa kwa kesi zinazohusiana na ukatili na udhalilishajiwa kijinsia, pamoja na kuongezeka kwa hukumu ambazo Mahakama zinaweza kupitisha. Kwa mfano, katika Mahakama ya Mkoa kesi za ukatili na udhalilishaji wakijinsia kutoka miaka 7 hadi miaka 14 na kwa Mahakama Kuu kutoka miaka 30 hadikifungo cha maisha.

**Kwa Ufafanuzi Zaidi Tafadhali Wasiliana na:**

**OFISI YA MTAKWIMU MKUU WA SERIKALI**
Sanduku la Barua,2321,
Simu: +255242231869
Barua pepe: cgs@ocgs.go.tzWebsite:
http://www.ocgs.go.tz

**MAKAO MAKUU YA POLISI ZANZIBAR**
Sanduku la Barua, 237,
Barua pepe:cidphqznz@gmail.comNukushi:
024223136
**MMP, Zanzibar.**